



## TAARIFA KWA UMMA

### **KUHUSU MWANGA COMMUNITY BANK LIMITED, EFC MICROFINANCE BANK (TANZANIA) LIMITED NA HAKIKA MICROFINANCE BANK LIMITED**

Kwa mujibu wa Kifungu cha 30(1)(a) na (b) cha Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, Benki Kuu ya Tanzania iliidhinisha Mwanga Community Bank Limited kuchukua umiliki wa EFC Microfinance Bank (Tanzania) Limited kuanzia tarehe 12 Septemba 2019. Pia, Benki Kuu ya Tanzania iliidhinisha kuunganishwa kwa Mwanga Community Bank Limited na Hakika Microfinance Bank Limited na kuunda benki ya huduma ndogo za Fedha inayojulikana kama Mwanga Hakika Microfinance Bank Limited mnamo tarehe 7 Januari 2020. Lengo la kuunganisha benki hizi ni kuongeza ufanisi katika utendaji na uzingatiaji wa sheria na taratibu za uendeshaji wa biashara ya kibenki.

Kufuatia idhini ya kuunganishwa kwa benki hizi, Benki Kuu ya Tanzania ilitoa leseni kwa benki mpya ya Mwanga Hakika Microfinance Bank Limited mnamo tarehe 30 Julai, 2020 na kufuta leseni za benki za Mwanga Community Bank Limited, Hakika Microfinance Bank Limited na EFC Microfinance Bank Limited. Hivyo basi, mali, madeni, wateja na wafanyakazi wa benki zilizofutiwa leseni vimehamishiwa kwenye benki ya Mwanga Hakika Microfinance Bank Limited.

Benki Kuu ya Tanzania inapenda kuwahakikishia wananchi kwamba itaendelea kusimamia kikamilifu taasisi zote za fedha nchini kwa lengo la kulinda maslahi ya wenye amana na kuhakikisha kwamba sekta ya fedha inaendelea kuwa salama na thabiti.

Kwa ufafanuzi zaidi kuhusu tangazo hili wasiliana na Mkurugenzi wa Usimamizi wa Sekta ya Fedha, Benki Kuu ya Tanzania, Namba ya Simu: +255 22 2235483, Nukushi +255 22 2234189 au Barua pepe - [DFSS\\_MANAGEMENT@bot.go.tz](mailto:DFSS_MANAGEMENT@bot.go.tz).

**BENKI KUU YA TANZANIA**

**25 Agosti 2020**